# Je, Uamuzi wa Kutumia Kiswahili Mahakamani Unatosha Kuleta Haki?

*Antoni M. Keya*[*]

**Ikisiri**

*Makala haya ni mwitikio kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuonyesha kukijali zaidi Kiswahili na hatimaye Bunge kupitisha Mswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2021 kukifanya Kiswahili kiwe lugha ya sheria na maswala yote yahusianayo na utoaji wa haki nchini. Mbali na kupongeza upandishaji ngazi Kiswahili, makala haya hujaribu kusema kwamba kukipandisha Kiswahili peke yake hakutapunguza ugumu wa lugha ya sheria, na hakutatufikisha kwenye hatua ya muhimu zaidi, mgawanyo sawa wa rasilimali lugha kati ya wakili na shahidi wakati wa mahojiano-bomozi. Makala haya yanapendekeza mapitio ya tafsiri zilizokwishafanywa kwa kuzingatia kwamba tafsiri za kisheria ni tofauti na nyinginezo; ianzishwe kampeni ya lugha rahisi ya kisheria kwenye makala yote ya kisheria; itafutwe njia ya kulainisha mahusiano kati ya sheria, haki na jamii au umma wa Watanzania. Mwisho, makala haya hupendekeza mfumo wa sheria wa advesaria utazamwe karibu pamoja na ule wa inkwizitoria ili kuona jinsi inavyoweza kupatikana njia nzuri ya kutoa au kuchukua ushahidi ambayo itazingatia mgawanyo wa rasilimali lugha.*

**Dhana za msingi:** *Advesaria, haki, inkwizitoria, Kiswahili, mahakama, sheria, Tanzania*

## Abstract

*This paper is a follow up to the Government of Tanzania's recognition of Kiswahili and the ensuing Written Laws Miscellaneous Amendment Act of 2021 to declare Kiswahili as the language of laws in the country and the language to be used in administration and the dispensation of justice. While acknowledging the importance of the declaration, this paper argues that this declaration alone will not make legal language any less difficult, and will not get us to the equitable distribution of discourse resources between councel and witnesses at cross-examination, which is a more pressing problem. The paper suggests a review of the legal translation of the already 'translated' documents, mounting a serious plain legal language campaign for the judiciary; making the relations between the law, justice and the Tanzanian public more cordial; and lastly, the paper suggests a closer look at the Adversarial Judicial System together with some elements of the Inquisitorial Judicial System to bring the equitable distribution of discourse resources during the evidence stage.*

[*] Senior Lecturer, Department of Foreign Languages and Linguistics, Unversity of Dar es Salaam, P.O. Box 35040, Dar es Salaam, Tanzania, E-mail: amkeya@yahoo.com

## Utangulizi

Mwezi Februari mwaka 2021 Tanzania ilishuhudia Kamati ya Bunge ikipitisha Mswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa 2021 ili kukiondoa Kiingereza kuwa lugha ya sheria na kukichagua Kiswahili kama lugha ya sheria chini. Kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania, Ibara ya 97 fasili ya kwanza bunge limekwishapeleka mswada huu kwa rais akatie saini yake kuufanya sheria. Tukio hili lilitokea majuma machache tu baada ya rais kumpandisha cheo Jaji Galeba kutoka Mahakama Kuu kwenda Mahakama ya Rufaa kwa sababu alikuwa 'amethubutu' kuandika na kutoa hukumu kwa lugha ya Kiswahili.

Kwetu wote ambao tumekuwa daima na maswali ya uchaguzi wa lugha (ama Kiswahili au Kiingereza) na matumizi ya rasilimali lugha katika kuwasiliana mahakamani tunapaswa kuipongeza serikali kwa kutia kibiriti kwenye utambi juu ya suala la matumizi ya Kiswahilimahakamani, kama njia mojawapo ya kufikisha haki kwa Mtanzania aliyekuwa kanyimwa nafasi ya kuyaelewa maamuzi yatolewayo juu yake mahakamani. Umuhimu wa maamuzi haya ni kama ilivyoelezwa kiufasaha kwenye kurasa 6 za mwanzo za Maombi ya Marejeo namba 23 ya 2020 Baina ya North Mara Gold Mine Ltd(Mwombaji) dhidi ya Gerald Nzumbi (Mjibu Maombi), yaliyotolewa Mahakama Kuu ya Tanzania, Divisheni ya Kazi, Musoma Mjini, yaliyotolewa kwa Kiswahili tarehe 22 Januari 2021 na Mheshimiwa Jaji Z, N Galeba. Kitendo hiki huleta fikira na ushawishi kwamba serikali ya Tanzania imeamua kuyavulia nguo maji juu ya suala zima la haki za raia zinavyoweza kupatikana kupitia mahakamani. Kwa ajili hii makala haya yanalitazama suala hili katika uzito mkubwa, kwamba hatimaye itaweza kusonga mbele zaidi ya kuchagua kutumia Kiswahili kama lugha ya mahakama.

Kwa mwelekeo anaoonyesha Ismail, kwenye jedwali la lugha za kuandika sheria, Kiswahili hakiingii sasa kama kitu kigeni. Kiswahili kimekuwa kikitumika kuandika "sheria mama (miswada), uandishi wa sheria nyinginezo, majadiliano ya miswada bungeni, upitishwaji wa sheria mama (kanuni na katiba), utungwaji wa kanuni (matangazo ya serikali), na tafsiri za sheria mama" (Ismail, 2020:14). Kwa hiyo labda Wizara ya Sheria na Katiba au waandaaji wengine hawatakuwa na Kiingereza wanachohitaji kupeleka kwenye Kiswahili ambacho hakina tafsiri yake tayari. Baadhi ya sheria na maandiko yaliyokwishatafsiriwa ni:

> (a). Kitabu cha Sheria kwa Kiswahili juzuu 1. (Kitabu hiki kina sheria za ndoa, mirathi, wasia na watoto wa kambo); (b). Kitabu cha Sheria za Barabarani, (Kitabu hiki kina sheria na kanuni za usalama barabarani) (2008); (c). Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (Sura ya 20); (d). Sheria ya Ardhi ya Vijiji (Sheria Namba 5 ya mwaka 1999); (e). Kanuni ya Adhabu (Sura ya 16); (f). Kiongozi cha Sheria, (Toleo la 5), kimetolewa na kituo cha msaada wa sheria kwa wanawake; (g). Sheria ya ndoa na talaka, (2013), kimetolewa na kituo cha msaada wa sheria kwa wanawake. Machapisho mengine yaliyopo kwenye mfululizo huu ni:
>
> (a). Makosa ya kujamiiana (b). Ugawaji mirathi kisheria (c). Haki na wajibu kati ya mume na mke (d). Kuishi kinyumba bila ndoa (e). Haki ya mtoto wa kambo kisheria (f). Kutelekeza mimba au motto (Ismail, 2020:16).

Mabadiliko haya yaliyokuja, kwa muonekano huo yanawagusa zaidi watoa maamuzi yaani majaji na mahakimu kwenye kuendesha mashitaka na kuandika hukumu. Ni vema kushikia hapa suala hili, na kujiuliza je, nia ya kuwasogezea na kuwapa watu haki kupitia mahakamani itatimia kwa hatua ya kubadilisha lugha ya mahakama peke yake?

Hebu tutazame hili suala kwa kupitia mambo yafuatayo: uchaguzi wa lugha dhidi ya matumizi ya rasilimali lugha; kinachoweza kutokea endapo tutaishia kwenye uchaguzi wa lugha tu (tena kwenye uandikaji wa hukumu); tunachopaswa kuzingatia juu ya tafsiri inayohitajika kwenye sheria na haja ya kampeni ya lugha rahisi; na haja ya kujenga mahusiano mazuri kati ya sheria, haki na jamii.

**Uchaguzi wa Lugha na Matumizi ya Rasilimali Lugha**

Tunaposema 'sasa tunatenda haki' ni njia nyingine ya kusema kwamba wakati mwingine hatutendi haki. Hali kadhalika tukisema 'acha/acheni haki itendeke' inaashiria kwamba haki ni kitu kinachotendeka kwa njia fulani kati mtu na mwenzie (Zipursky, 2005:134). Kutendeka au kutotendeka kwa haki kunaashiria kuwa haki ni sifa ambayo huweza kupatikana au kukosekana, wakati mwingine hata kucheleweshwa, labda ndiyo sababu tunayo maksimu mashuhuriya William Ewart Gladstone isemayo 'Justice delayed is justice denied'. Rawls husema kwamba vitu vingi tu vinaweza kuwa haki au batili, zikiwemo sheria, taasisi na mifumo ya jamii. Kwa

hiyo sheria iliyokuwa imekipa Kiingereza nguvu juu ya Kiswahili kwa 'faida ya Waswahili' ilikuwa batili, na Mswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa 2021 umekuja kama haki iliyokuwa ikingojwa. Baadhi ya matendo pia yanaweza kuwa ya haki au batili (mfano ni mfumo wa kufikia maamuzi) (Rawls, 2011:7). Matendo batili (yasiyo ya haki) kwa mlei hayamaanishi kwamba lazima yawe kinyume cha sheria husika. Hapa ndipo yanapokuja matumizi ya rasilimali lugha, ambayo ni halali kisheria lakini batili kwa mtendewa. Mfano ni mahojiano-bomozi yaani cross-examination ambapo kuna mipangilio na haki za kushiriki mazungumzo, yaani kati ya wakili na shahidi, nani anasema nini na kwa njia ipi, hali kadhalika. Katika mfumo wa advesariawakili huuliza maswali kwa njia inayomlazimisha shahidi kujibu anavyotaka wakili, hata kama ukweli sivyo ulivyo. Shahidi hapewi nafasi ya kutoa ufafanuzi wakati wa mahojiano kati yake na wakili. Makala nyingi za utafiti zinajikita kuchunguza raia anavyonyimwa haki hii mahakamani.

Kwa hiyo kwakuutazama mswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa 2021 wa kuondoa Kiingereza kama lugha ya sheria na badala yake kutumia Kiswahili, suala la kuchagua lugha moja kwenda nyingine litakuwa limekamilika. Haki ya kuona maandiko na kusikia sauti za Kiswahili zaidi mahakamani tutakuwa tumeipata. Lakini makala za kiuchunguzi kuhusu hali ya upatikanaji haki kupitia mahakamani Tanzania na nje ya Tanzania zinaonyesha kwamba suala la uchaguzi wa lugha peke yake (kama tulipofika sasa) halitoshi kusawazisha uwanja wa kuchezea, haliwezi kufanya haki itendeke ipasavyo. Makala ya Keya (2016:29-31) hujadili na kuonyesha ambavyo suala la lugha ya Kiswahili pekee halitoshi. Anaonyesha mfano wa shahidi ambaye kwa maneno ya Wazee wa Baraza anaonekama 'mwenye ushahidi wa kutunga' baada ya kutoa majibu yaliyoonekana kuchanganya neno 'amua' kati ya kumaanisha 'decide' (kata shauri) na 'stop the fight' (ingilia kati kufanya ugomvi uishe). Kumbe Kiswahili fasaha au hata Kiswahili cha sheria si lugha ya kila anayeongea Kiswahili. Jacquemet naye anasema kwamba mbali na kwamba ma-pentiti di camorra (waitaliano kutoka Camorra) huongea Kiitaliano, hushindwa kuwasiliana kiufasaha mahakamani Italia kwa kuwa wanategemea Kiitaliano wanachoongea mitaani. Anasema kwamba mapungufu ya lugha yanafanya wanaotoa maamuzi wawe na mtazamo hasi juu ya mashahidi (Jacquemet, 1992:113).

Kwa hiyo, kwa mswada ulioko mezani tutakuwa tumefaulu kuchagua lugha yetu wenyewe lakini matumizi ya rasilimali lugha

kwa Kiswahili kama ilivyo lugha nyinginezo tunaweza kuwa hatujafanikiwa. Haki hii, ambayo ni kubwa zaidi, tutakuwa hatujaifikia. Kwa upande huu, wakati wa mahojiano-bomozi wakili huruhusiwa kumbana shahidi ili atoe majibu fulani tu (Freedgood, 2002:5 na Magenau, 2004:39). Mfumo wa kisheria wa adversaria (adui au pinzani) humtaka wakili awe chonjo kuonyesha matobo kwenye ushahidi atoao shahidi (Parriag, 2001:9) na mahojiano-bomozi hulengwa kumshushua shahidi ili aonekane mwongo (Murphy, 2000:509), na ni "lazima apatikane mshindi" (Maley, 1994:33). Kwa njia hiishahidi na wakili wanatazamwa kama washindani (au maadui), mwamuzi akiwa hakimu au jaji. Tofauti ya ushindani huu na kandanda au mchezo mwingine, ni kwamba hapa mmoja, yaani wakili, kasomea anachofanya, na hakuna kigezo cha kielimu ili kuwa shahidi. Wakili yeye lazima awe na shahada ya sheria, mwaka wa Shule ya Sheria na mazoezi, yote kwa kazi hii. Kwa hiyo si suala geni 'wakili msomi' mwenye shahada ya umahiri au hata uzamivu kushindana na shahidi ambaye hajauona hata mlango wa darasa la shule ya msingi. Kwa kuwa 'lazima mshindi apatikane' (Maley, 1994:33) unadhani nani ana nafasi kubwa ya kushinda? Wakili anazijua vema zaidi kanuni za matumizi ya rasilimali lugha mahakamani. Yeye hufanya hii kama kazi yake ya kujipatia mkate wake wa kila siku. Ni mwenyeji. Kutokana na ushindani huu, wasomi wengi wametumia tashbiha tofauti kuuelezea. Maley (1994:32-3) na Kirchheimer (1969:342) huufananisha ushindani huu na vita ya uharakivu wa ubongo; Woodbury (1984:206) anaufananisha na shindano la kusimulia hadithi; na Drew (kama alivyonukuliwa na Freedgood, 2004:4) huufananisha na mchezo wenye madhara makubwa. Haya ni matumizi ya rasilimali lugha yalivyopangwa mahakamani chini ya mfumo huu wa sheria. Zikifanywa juhudi kuanzia hapa, tutakuwa kwenye barabara salama zaidi ya kuelekea kwenye haki katika matumizi ya rasilimali lugha.

**Kikiachwa Kilivyo, Kiswahili nacho Kitatutesa tu**

Mbali na kwamba sheria nyingine zimekwishatafsiriwa kutoka Kiingereza kuja Kiswahili, ningependa kuongelea ugumu kwa ujumla wa lugha ya sheria. Akijitahidi kuwaonyesha wajumbe wa Law Reform Commission ya Victoria jinsi Kiingereza cha sheria kilivyo kigumu kueleweka kwa wasio wanasheria na hata wanasheria wenyewe, Eaglesson alitumia uchambuzi wa kazi za kisanaa wa *Gulliver's Travels* (Jonathan Swift), na sinema mbili za *Animal Crackers* na *A Day at the Races* (Marx Brothers), pamoja na ukosoaji alioufanya Charles Dickens kwenye *Bleak House*

(Eaglesson, 1991). Wengineo walioiongelea mada hii, zamani kiasi, ni Bentham (1838), Mellinkoff (1963), na Renton (1975). Matatizo ya ugumu wa lugha ya sheria hayako kwenye lugha ya Kiingereza pekee. Duarte i Montserrat (1993) na Duarte i Montserrat na Martinez (1995) wanaonyesha ugumu wa lugha za Catalani na Kihispania kwenye sheria; Cavagnoli na Wölk (1997) huonyesha matatizo hayo hayo katika Kiitaliano. Gunnarsson (1984) huonyesha matatizo ya Kiswidi kitumikacho kwenye sheria; huku Okawara (2004) akionyesha jinsi Kijapani cha kisheria kilivyo kigumu kwa Wajapani wa kawaida. Hii huashiria kwamba hata Kiswahili kitatusumbua endapo mapinduzi hayatafanyika ama kutokea ndani au nje ya Mahakama au Wizara ya Sheria na Katiba. Mpaka sasa hatujawa na mkakati wowote bayana wa kujiepusha na matatizo yanayowasibu Waingereza, Waitaliano, Waswidi, Wakatalani, Wahispania, Wajapani na wengineo. Lakini baadhi yao, kwa hakika zaidi Waingereza na Wamarekani, wameshapiga hatua juu ya hili kupitia kampeni ya lugha rahisi ya sheria.

**Kutafsiri Sheria na Maamuzi ya Kesi**

Tunapoitazama mahakama au Wizara ya Sheria na Katiba na kazi mpya (ya 'kuhamia nyumbani') ya kutafsiri sheria na kutoa maamuzi katika lugha ya Kiswahili, tunahitaji kuzingatia yafuatayo. Kutokana na umaalum wa sheria, bila kujali lugha inayotumika, na muundo wa sheria husika, Fröhlich (2014: 117) anawanukuu Cao (2007) na Šarčević (2012) wakisema kwamba ukalimani wa sheria, yaani 'legal translation' ni ukalimani maalum na 'the most complex and demanding of all areas of specialized translation' ikiashiria kwamba si kila 'mkalimani' ataweza kufanya kazi hii. Ugumu huu huhitaji maarifa ya juu zaidi ya mkalimani kujua lugha au matini chanzi (L1) na lugha au matini lengwa (L2), lakini anapaswa kuwa na maarifa zaidi ya maneno moja moja yanachomaanisha, vifungu maneno na sentensi zinachomaanisha kisheria na athari za kisheria yaliyonayo (Fröhlich, 2014: 117).

Vile vile, lugha ya sheria ina (kwa kukosa maneno mepesi ya Kiswahili) "embeddings, subordinations, syntactic discontinuities, passive constructions, nominalizations, negations and archaic, complex prepositions or constructs" ambazo kila moja miongoni mwa wanasheria zina umuhimu wa kutoacha wazi mianya ya kujichanganya, ambazo ni vigumu kumkuta mkalimani anayejua sheria ameviruka. Hivyo vyote ni sehemu ya 'legalese' (uanasheria-sheria), ambazo Giampieri husema hufanya lugha ya kisheria isieleweke kwa asiye mwanasheria (Giampieri, 2016: 424). Ni vema

kusisitiza kwamba kutafsiri kazi ya kisheria si mchezo (Moreno, 2016:100). Ni sifa hizo zinazofanya hata Kiswahili cha sheria kiwe kigumu miongoni mwa waswahili. Kazi ya kupambana na sifa hizi inaambatana na kuendana na kipengele kifuatacho hapa chini.

**Kutafsiri na Kampeni ya Lugha Rahisi**

Ufasiri wa mambo ya kisheria unahitaji umakini mkubwa kuutekeleza. Njia sahihi (labda si rahisi) ni kulenga kuiweka sheria katika maneno rahisi yaliyo wazi zaidi kwa mtu wa kawaida. Tunachohitaji hapa ni kuunga mkono kwa vitendo au kuanzisha kampeni ya kuzichambua istilahi za kisheria kuona sehemu zinapoweza kusababisha ugumu wa kimawasiliano. Kampeni hii kwingineko huitwa 'plain language movement'. Kampeni ya 'plain language' ilianzishwa na andiko la Gowers mwaka 1948 na 1954 nchini Uingereza. Huko Marekani kampeni hii ilitiwa saini na rais Jimmy Carter. Makala ya Penman (1992) pia ni nzuri juu ya mada hii. Hatua hii ni muhimu kuifanya kwani vinginevyo tunaweza kufanya ukalimani unaowatenga walio wengi wasio ndani ya kundi la 'wasomi' na hivyo juhudi ya serikali ya kusogeza haki kwa wengi kupotea. Wanaoteseka zaidi ni wale ambao hawajasoma kabisa, ambao hukadiriwa kuwa asilimia 7 katika nchi nyingi, na ndio wengi wao hushtakiwa kwa makosa ya jinai (Hayes, 1993).

**Kujenga Mahusiano Mazuri kati ya Sheria, Haki na Jamii**

Kuna haja pia ya kuoanisha au kujenga urafiki wa kweli kati ya *sheria, haki* na *jamii* ya Kitanzania. Uhusiano uliopo kati ya sheria na jamii hutazamwa na wasomi kwa njia mbili: 'formalism' na 'instrumentalism'. Formalists huitazama sheria kama muundo unaojitosheleza na kujifungia mipaka, kwamba maendeleo yake huweza kuelezwa vema na wale pekee walio ndani ya kundi (Bourdieu, 1987:814). Yaani kwamba ni mfumo uliojitenga na hauihitaji jamii ya nje ili kuelezeka au kutenda kazi. Hazard husema kuwa fani ya sheria kwa kujitofautisha na makundi mengine, imejiwekea mipaka ya kazi zao, hujipa utambulisho wao na kudumisha fani yao kama kundi huru kwenye jamii (Hazard, 1991:1240-1241). Ndivyo hivi sheria na Mahakama ya Tanzania ilivyo au inavyoonwa na jamii inayogonga hodi kila siku kuhudumiwa. Kwa namna hii hakuwezi kuwa na urafiki kati ya sheria na wanajamii kwa sababu wanasheria wamejifungia kama fani iliyojitosheleza.

Instrumentalists wao wanatazama sheria kama akisi ya mahusiano yaliyopo katika jamii, ambapo matakwa ya jamii tawala hujionyesha (Bourdieu, 1987:814). Hivi ni karibu kiasi na Mahakama ya Tanzania inavyostahili kuwa au kuonekana machoni mwa wanajamii. Ufasiri wa sheria na maandiko mengine ya mahakama unapaswa kuakisi hata katika lugha yake, kuanza kuondoka kwenye 'formalism' kuelekea kwenye 'instrumentalism'. Wasomi wengi wamechunguza jinsi kutafsiri maana za kisheria kunavyoleta msigano mahakamani kati ya wasio wanasheria na wanasheria. Nyingi ya stadi hizi (mf. Beach, 1985; Danet, 1980; Dunstan, 1980; Goodman *na wenzie.,*1998; Hale & Gibbons, 1999; Konradi, 1996; Luchjenbroers, 1991; Matoesian, 1993; Penman, 1987; Rigney, 1999; Wahn & Clayton, 1996; Walker, 1987 na Keya, 2013) huonyesha kwa viwango tofauti jinsi ambavyo mahojiano-bomozi huonyesha kutokuwapo urafiki kati ya wanasheria dhidi ya waitwao walei, ambao ndiyo jamii inayoitegemea mahakama kutatua migogoro yao ya kisheria. Unaoonekana ni utengano badala ya muungano. Nyingi ya makala haya yanatokana na tafiti kwenye jamii zinazofuata mfumo wa sheria inaofuata Tanzania.Mahakamani mashahidi hukosa uhuru kwani wanabanwa wanapojaribu kutafuta nafasi ya kujieleza tofauti ya matakwa ya muundo wa mahakama (Keya, 2013; Keya, 2016; Keya, 2017a; Keya, 2017b).

Mapinduzi yanayopaswa kufanyika kutokea ndani ama nje ya mahakama ni kubadili mtazamo wa jinsi mahakama inavyotazamwa na kujiuliza faida ya kufuata mfumo huu wa sheria (uadvesaria) badala ya mfumo wa inkwizitoria. Ufasiri unaopaswa kufanyika unapaswa kutazma mbali na utamaduni wa kundi la wanasheria ambao kwa mujibu wa Bourdieu hujichukua kama kundi pekee (1987: 814)na wenye hamu ya kukuza utamaduni wa kisheria (Bogoch 2000: 227).Lakini kwa kuwa lengo la kuwa na sheria, kwa mujibu wa Zipursky, lilikuwa kuboresha mahusiano na furaha ya jamii kwa kuwafidia walioonewa na kuboresha ustaarabu wa jamii (Zipursky, 2005:128), na kwa kuwa sheria iliwekwa na wenye mamlaka ili iwasaidie wasio na mamlaka (Shivji*na wenzie,* 2004:7), ni muhimu tuhakikishe kwamba sheria yetu inawafaa hata walio chini kiuwezo.

## Mjadala na Hitimisho

Mtu anayejali kiu ya haki ya Watanzania akiuliza endapo Watanzania watakuwa wamefanikiwa kusogeza haki kwa hatua jasiri ya kuondoa Kiingereza kama lugha ya Mahakama na kupandisha Kiswahili, jibu la makala haya ni "Hapana, ila safari

inaweza kuwa imeanza vizuri". Tumethubutu kuyanyonga mawazo na kufuta nyayo za mtawala wetu wa zamani ambaye alitugawia lugha ya Kiingereza mahakamani na hata mfumo wa sheria. Sidhani kwamba kwa hatua hii serikali imetania. Itakuwa bahati mbaya sana endapo hakutakuwa na lolote zaidi ya Watanzania kusikia na kusoma wenyewe hukumu za Kiswahili. Kwa mswada huu, bado tunahitaji kupunguza ugumu wa lugha ya sheria. Tunahitaji kufanya kampeni ya lugha rahisi ya sheria; na tunahitaji kujenga ukaribu zaidi kati ya sheria, haki na jamii.

Gibbons husema kwamba mahala Kiingereza kinapotumika kama lugha ya sheria (mahakama) kama ilivyokuwa hapa Tanzania, mfumo wa advesaria ndio mfumo unaotumika (Gibbons, 2003:5). Kwa mtazamo huu, hapa tulipo sasa na Kiswahili chetu tutafuata mfumo gani wa sheria? Hii inaashiria pia kwamba hatua tuliyokwishapiga, tunaweza kupiga zaidi. Tunaweza kujiuliza maswali magumu kuhusu mfumo wa sheria tulio nao, kwa sababu nao pia kama kilivyokuwa Kiingereza uliachwa na watawala wakoloni. Suala la utoaji ushahidi mahakamani (kwenye ugawaji rasilimali lugha) linasumbua zaidi kuliko suala la ama Kiingereza au Kiswahili. Kwa nini tusipige hatua zaidi?

Utofauti wa hatua ya kwanza tuliyopiga kuhusu Kiswahili na hii ya kurekebisha matumizi ya rasilimali lugha ni kwamba hili la pili inabidi kwanza lionekane na 'wengi' kuwa ni shida, liandikiwe vya kutosha, hatimaye kisiasa liandamaniwe na kubebewa mabango. Kwa sasa bado linaweza kuonekana kama ni suala la madarasani na shauku ya wachache. Msigano katika kutumia rasilimali lugha upo, umeganda vichwani mwa Watanzania waliokwishahudhuria mahojiano kwamba 'suala hilo liko hivyo hivyo' kwamba ni wao wenyewe ndio wanaostahili kubadilika kufuata muundo (Keya, 2013). Watanzania wengi walio nje ya jamii ya wanasheria hawajui kwamba kuna njia nyingine tofauti na barabara wasafiriayo. Mbali na hiyo, hii hatua ya pili haiwezi kwenda kirahisi kama hatua ya kwanza ilivyokwenda. Hii inahitaji mafunzo upya juu ya mfumo wa sheria wa inkwizitoria ambao unahitaji kufuatiliwa kuanzia hatua ya chini kiasi. Mfumo huu unamtwisha mzigo zaidi jaji.

Tofauti kubwa kati ya mifumo hii miwili ya sheria ni kumchukulia mtuhumiwa kwamba si mkosaji mpaka itakapothibitika hivyo, yaani 'presumption of innocence' na majukumu ya washiriki, hasa mawakili na majaji.  Lakini pia kunaweza kukawa na uamuzi wa kuchanganya sehemu za hii mifumo miwili. Kwa mfano, "China na

Japan wamefanya mchanganyiko wa njia za kijamii za kutatua migogoro na aina nyingine ambazo zinafanana na kufuata mfumo wa inkwizitoria. Wajapani wao waliamua kuchukua muundo mzima wa Kijerumani. Wachina hufuata inkwizitoria kwa masuala ya jinai na advesaria kwa Sheria ya Mikataba" (Gibbons, 2003:4). Makala haya hupendekeza mabadiliko kwenye ukusanyaji wa ushahidi pale wanapopambanishwa wanandondi wasio na uzito sawa, na nafasi ya jaji hapa ipewe mashiko zaidi, awe hasa zaidi ya mwamuzi.

Mwisho, tulenge kuitazama mahakama kama mwakilishi wa jamii katika kutekeleza haki si kwa ajili yake yenyewe, ila kwa ajili ya kila mwanajamii (Kenny, 1999), na kusisitiza kwamba mamlaka ya mahakama yatokane na imani ya jamii kwa utendaji wa mahakama. Yaani jukumu la mahakama liwe kutatua migogoro miongoni mwa wananchi (wao kwa wao) na wananchi na serikali yao kwa mujibu wa sheria, ambapo sheria yenyewe inatokana na jamii (Zdenkowski, 2007).

Wanasheria wanakijua na kukielewa vema kitendo hiki, ambacho Rawls na wadau wa ugawaji wa rasilimali lugha tunaona ni haki ya msingi sana inayopotea. Ni vema tuwasaidie wanasheria wetu kuelewa au kukumbuka kwamba kitendo wanachofanya ni batili japokuwa kinakubalika kisheria. Wanasheria wanafahamu vema kinachotokea kuhusu mgawanyo wa rasilimali lugha, lakini husema, "ndivyo ilivyo, kwa mfumo huu inapaswa kuwa hivyo"; wananchi wanasema, "ndivyo ilivyo, inabidi tu". Kila upande ukisema, "ndivyo ilivyo" hakutakuwa na uthubutu, hakuna kitakachobadilika. Serikali imekataa kukubali tu kwamba "ndivyo ilivyo", na sasa tuna Kiswahili kama lugha ya mahakama. Tuendelee kuwaza na kusema tofauti na mazoea. Tupige hatua zaidi.

## Marejeleo

Beach, W. (1985). Temporal Density in Courtroom Interaction: Constraints on the Recovery of Past Events in Legal Discourse. *Communication Monographs*, 52: 01–19.

Bentham, J. (1838). *The Works of Jeremy Bentham,* ed. J. Bowring. Edinburgh: William Tait.

Bogoch, B. (2000). Discourse Dilemmas and Courtroom Control: the Talk of Trial Judges. *Law & Social Inquiry*, 25(1): 227–247.

Bourdieu, P. (1987). The Force of Law: Toward a Sociology of the Juridical Field. *The Hastings Law Journal,* 38: 805–853.

Cavagnoli, S. & Wölk, J. (1997). *Einfuhrung in die Italienische Reschssprache-Introduzione all'italiano Giuridico.* Munich/Vienna/Bern: Bern/Manz/Stampf.

Danet, B. (1980). Language in the Legal Process. *Law & Society Review*, 14: 445–564.

Duarte i Montserrat, C. (1993). *Llengua i Adminiustraci'o.* Barcelona: Columna Edicions.

Duarte i Montserrat, C. & Martinez, A. (1995). *El Lenguaje Juridico.* Buenos Aires: A-Z editora.

Dunstan, K. (1980). Context for Coercion: Analyzing Properties of Courtroom "Questions". *British Journal of Law and Society*, 7(1): 61–77.

Freedgood, L. (2002). Voicing the Evidence: The Pragmatic Power of Interpreters in Trial Testimony. A PhD Thesis, Boston University.

Fröhlich, L. (2014). Legal Translation: A Study of Rogatory Letters and its Implications. *Language and Law,* 1(2): 117–119.

Giampieri, P. (2016). Is the European Legal English Legalese-Free? *Italian Journal of Public Law,* 8(2): 424–440.

Gibbons, J. (2003). *Forensic Linguistics: An Introduction to Language in the Justice System.* Cornwall: Blackwell.

Goodman, G. S., Tobey, A. E., Batterman-Faunce, J. M., Orcutt, H., Thomas, S., Shapiro, C. & Sachsenmaier, T. (1998). Face-to-face Confrontation: Effects of Closed-circuit Technology on Children's Eyewitness Testimony and Jurors' Decisions. *Law and Human Behavior*, 22(2): 165–203.

Gowers, E. (1948). *Plain Words.* London: Her Majesty's Stationery Office.

Gowers, E. (1954). *The Complete Plain Words*. London: Her Majesty's Stationery Office.

Gunnarsson, B. L. (1984). Functional Comprehensibility of Legislative Texts: Experiments with a Swedish Act of Parliament. *Text,* 4(1–3): 71–105.

Hahn, P. & Clayton, S. (1996). The Effects of Attorney Presentation Style, Attorney Gender and Juror Gender on Juror Decisions. *Law and Human Behavior*, 20: 533–554.

Hale, S. & Gibbons, J. (1999). Varying Realities Patterned Changes in the Interpreter's Pepresentation of Courtroom and External Realities. *Applied Linguistics,* 20(2): 203–220.

Hayes, S. (1993). *People with an Intellectual Disability and the Criminal Justice System: Appearances before Local Courts* (4). Sidney: New South Wales Law Reform Commission.

Hazard, G. C. (1991). The Future of Legal Ethics. *The Yale Law Journal*, 100(5): 1239–1280.

Ismail, J. (2020). Mchango wa Tasinia ya Sheria katika Ukuzaji na Uenezaji wa Kiswahili Tanzania: Mifano kutoka Mahakama ya Tanzania na Taasisi za Wadau wa Sheria. *East African Journal of Swahili Studies*, 2(2): 11–22.

Jacquemet, M. (1996). *Credibility in Court: Communicative Practices in the Camorra Trial.* Cambridge: Cambridge University Press.

Kenny, S. (1999). Maintaining Public Confidence in the Judiciary: A Precarious Equilibrium. *Monash University Law Review,* 25(2): 209.

Keya, A. (2013). *A Critical Discourse Analysis of Cross-Examination at the High Court of Tanzania in Dar es Salaam.* PhD Dissertation, University of Dar es Salaam.

Keya, A. (2016). "Nani Aliamua?" Sera ya Lugha na Kitokeacho Mahakamani Tanzania. *Journal of Linguistics and Language in Education,* 10(1): 20–36.

Keya, A. (2017a). The Counsel-Witness Battle of Identities on Cross-Examination at the High Court of Tanzania in Dar es Salaam. *Journal of Linguistics and Language in Education,* 11(1): 1–18.

Keya, A. (2017b). How Some Witnesses Have Vied for Floor Control in Tanzanian Higher Courts. *Tanzanian Journal of Population Studies and Development*, 24(1&2): 94–107.

Kirchheimer, O. (1969). *Political Justice – The Use of Legal Procedure for Political Ends*. Princeton, NJ: Princeton University Press.

Konradi, A. (1996). Preparing to Testify: Rape Survivors Negotiating the Criminal Justice process. *Gender and Society*, 10(4): 404–432.

Luchjenbroers, J. (1991). Discourse Dynamics in the Courtroom: Some Methodological Points of Description. *La Trobe University Working Papers in Linguistics*, (4): 85–109.

Magenau K. S. (2003). Jury Duty: Competing Legal Ideologies and the Interactional Negotiation of Authority in Jury Deliberation. PhD Thesis, Georgetown University.

Maley, Y. (1994). The Language of the Law. In J. Gibbons (ed.). *Language and the Law*. London: Longman.

Matoesian, G. M. (1993). *Reproducing Rape: Domination through Talk in the Courtroom.* Chicago: Chicago University Press.

Melinkoff, D. (1963). *Language of the Law*. Boston, M.A: Little, Brown.

Moreno, F. J. (2016). V- Teaching the Use of ad hoc Corpora. *Language and Law/Linguagem e Direito*, 3(1), 100–119.

Murphy, P. (2000). *Murphy on Evidence* (7th Edition). London: Blackstone Press Limited.

Okawara, M. H. (2004). Legal Japanese Viewed the Unfair Competition Prevention Law. In J. Gibbons, V. Prakasham and K.V. Tirumalesh (eds.). *Justice and Language*. Delhi: Longman Orient.

Parriag, A. (2001). An Analysis of Courtroom Dynamics of Sexual Assault Trials. PhD Thesis, Carleton University.

Penman, R. (1987). Discourse in Courts: Cooperation, Coercion and Coherence. *Discourse Processes,* 10: 201–218.

Penman, R. (1992). Plain English: Wrong Solution to an Important Problem. *Australian Journal of Communication,* 19(3): 1–18.

Rawls, J. (2011). *A Theory of Justice.* New Delhi: Universal Law Publishing.

Renton, D. (1975). *The Preparation of Legislation: Report of a committee appointed by the Lord President of the Council.* London: Her Majesty's Stationery Office.

Rigney, A. C. (1999). Questioning in Interpreted Testimony. *Forensic Linguistics*, 6(1): 1350–1771.

Shivji, I., Majamba, H., Makaramba, R., & Peter, C. (2004). *Constitutional and Legal System of Tanzania: A Civics Sourcebook.* Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers Ltd.

Wahn, P. & Clayton, S. D. (1996). The Effects of Attorney Presentation Style, Attorney Gender and Juror Gender on Juror Decisions. *Law and Human Behavior*, 20(5): 533–554.

Walker, A. G. (1987). Linguistic Manipulation, Power and the Legal Setting. In L. Kedar (ed.) *Power through Discourse.* New Jersey: Ablex.

Watson, A. (2007). Law and Society. In J. W. Cairns and P. du Plessis (eds.) *Beyond Dogmatics: Law and Society in the Roman World.* Edinburgh: the Edinburgh Law Review Trust and the Contributors.

Woodbury, H. (1984). The Strategic Use of Questions in Court. *Semiotica*, 48(3/4): 197–228.

Zdenkowski, G. (2007). *Magistrates' Courts and Public Confidence.* Canbera: NSW Local Courts.

Zipursky, B. C. (2005). Philosophy of Tort Law. In M. P. Golding and W. A. Edmundson (eds.). *The Blackwell Guide to the Philosophy of Law and Legal Theory.* Oxford: Blackwell Publishing.